**Mt. Marko Mwinjili na Msimamizi wa Parokia**
*Aliishi Yerusalemu. Baada ya ubatizo wake, akafuatana na Mtume Paulo. Kisha aliishi Roma na Mt. Petro, akaandika Injili akikusanya mafundisho yake. Akaeneza Ukristu na kuanzisha Kanisa Aleksandria ya Misri. Akawa Mhubiri, Askofu na Shahidi wa kwanza kwenye bara la Afrika.*

**Gazeti la Parokia Katoliki**
**ya Mtakatifu Marko Mwinjili ya Ol Moran**
*N. 84 — Mwaka wa 14*
**Aprili 2022**

# SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO

*Silver Jubilee 1997-2022: Parokia yatimiza miaka 25*

## Shukrani na Baraka

Januari tarehe 1, mwaka 1997: Parokia Katoliki ya Ol Moran ilianzishwa na Askofu Mkuu wa Nyeri, Nicodemus Kirima, ikapata jina la Msimamizi Mtakatifu Marko Mwinjili. Iligawiwa kutoka Parokia ya Familia Takatifu ya Ng'arua, alipokuwa Paroko Fr. Sandro Borsa. Mwanzilishi wa Parokia na Baba Paroko wa kwanza wa Ol Moran akawa Fr. Giovanni Volpato, Padri Mmishonari wa Jimbo la Venisi (Italia). Ndiyo sababu tangu mwanzo Parokia imekuwa na ufadhili wa pekee wa Jimbo la Venisi pia. Hapo mwanzo Makanisa Madogo yalikuwa Mithuri, Kabati, Minjore, Githima, Gituamba, Kahuho, Ol Moran, Magadi, Miharati, Lounyek.

> Tufanye Shukrani tukikumbuka mambo yaliyopita; tuombe Baraka tukijitolea kwa kazi za Kanisa siku za usoni.

Tangu mwaka 2003, Jimbo Katoliki la Nyahururu lilipoanzishwa, Ol Moran imekuwa chini ya Askofu wa Nyahururu: kwanza Luigi Paiaro, baadaye Joseph Mbatia.

Kwa maneno machache, mambo haya ni mwanzo wa Parokia ya Ol Moran. Tangu wakati ule, mambo mengi yalifanyika, kwa muda wa miaka 25. Ndiyo sababu mwaka huu tumeamua uwe mwaka wa sherehe: tukikumbuka yaliyopita, mazuri kwa mabaya, tumfanyie Mungu shukrani! Zaidi ya hayo, tunawakumbuka watu wengi waliofanya kazi katika Parokia hii au pamoja na sisi: Mapadri, Masista, Makatekista, Viongozi, Wakristu, wafadhili na marafiki.

Hivyo, tunatambua vile Mungu alivyotaka kuja karibu nasi na kutengeneza kati yetu sehemu ya urithi wake. Alisema agano lake: "Mimi nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu wangu". Naye amekuwa mwaminifu!

Kusherehekea miaka 25, lakini, siyo sababu ya kumbukumbu peke yake. Ni nafasi nzuri ya kutazama mbele pia: kazi iliyoanza haijakamilika bado. Lazima Ufalme wa Mungu utangazwe bado katika eneo hili, na uendelee kukua. Injili ya Kristu izidi kuhubiriwa kwa ajili ya jamii na familia za Ol Moran. Nani ataendelea na kazi hii? Nani atajitolea katika wajibu huu? Ni wakati wetu, sisi tumetumwa sasa: ndipo katika Sherehe ya Silver Jubilee tunamwomba Mungu baraka ya pekee, tuwe na nguvu ya kufanya kazi za Kanisa siku za usoni.

Fr. Giacomo Basso - *Baba Paroko*

25
1997—2022 Silver Jubilee

**SAINT MARK** CATHOLIC PARISH - Ol Moran
*Catholic Diocese of Nyahururu*

**SILVER JUBILEE**
**1997-2022**

Ever present
in your midst,
I will be your God,
and you will be
my people.
(Lv 26:12)

*Sherehe zinaendelea mwaka mzima*

# Silver Jubilee: miaka 25 ya Parokia

MPANGO WA MWAKA na KALENDA
Kumbukumbu ya Miaka 25 ya Parokia haitakuwa ya siku moja tu, bali inaendelea mwaka huu wote na sherehe na kazi mbalimbali.
Hata Kalenda ya mwaka huu imeundwa na picha mbalimbali za historia ya Parokia.

KUMBUKUMBU YA MWANZO WA PAROKIA *(Januari)*. Tarehe 1 Januari waakilishi wa viongozi na Makatekista walikuwa pamoja katika Ibada ya Mwanzo wa Mwaka, wakikumbuka siku yenyewe ya mwanzo wa Parokia, 1 Januari 1997. Tena, Jumamosi 22 Januari, Viongozi wote walikutana pamoja katika Parish Assembly ya 16.

MASOMO KATIKA MAKANISA (*Kwaresima, Mwezi wa tatu).* Katika kipindi cha Kwaresima, Walimu wa *Pastoral Teams* wametembelea Makanisa Madogo yote wakiwapatia Wakristu masomo maalum kuhusu *Silver Jubilee* na kuhusu maana yake ya kiroho.

**MPANGO WA SIKU YA SHEREHE**

09.30am: *Kupandisha Bendera za Kitaifa*

10.00am: *Misa ya Sherehe ya Mt. Marko Mwinjili, inayoongozwa na Baba Askofu Joseph, pamoja na Mapadri wa Parokia na Mapadri waliohudumu Ol Moran. Katika ibada kutakuwa na Nadhiri za CMA na CWA. Mwishoni mwa Misa kutakuwa na utenzi wa Mtakatifu Marko.*

12noon: *Maongeo na Zawadi*

12.30pm: *Baraka ya mradi wa Parokia, kujenga Jukua uwanjani nyuma ya Kanisa.*

01.00pm: *Maburudisho na Ngoma za Kitamaduni*

02.00pm: *Chakula cha mchana*

SHEREHE YA SILVER JUBILEE *(Jumamosi 30 Aprili)*. Hiyo itakuwa ile sherehe yenyewe ya Silver Jubilee, tukisherehekea miaka 25 ya Parokia, pamoja na Baba Askofu, Mapadri waliohudumu Ol Moran, na marafiki wengine. Hata Fr. John Volpato atakuja kututembelea. Siku hiyo, wanachama wa CMA na CWA watafanya Nadhiri zao za mwaka huu.



MRADI WA JUKUA. Siku ya Sherehe itakuwa pia nafasi ya kuanzisha mradi wa Parokia wa kukumbuka Silver Jubilee, yaani kujenga Jukua la kudumu katika uwanja nyuma ya Kanisa, kwa ajili ya ibada zinazoadhimishwa nje, na kwa ajili ya kazi na sherehe nyinginezo.

BARAKA DAY *(Mei-Juni)*. Baada ya Sherehe kutakuwa na siku za Baraka Day katika Makanisa Madogo. Sadaka ambazo Wakristu watatoa kwa Baraka Day zitachangia mradi wa Jukua.

HARAMBEE *(Julai)*. Kwa kuchangia mradi wa Ujenzi wa Jukua, viongozi wameanza kupanga siku maalum ya mchango: itakuwa Jumapili 3 Julai. Mpango kamili wa Harambee utatangazwa baadaye, wakati ufaao.

JUBILEE YA NDOA *(Jumamosi 5 Novemba)*. Kwa kumalizia sherehe zote za Silver Jubilee, mwezi wa kumi na moja kutakuwa na siku ya Jubilee ya Ndoa, yaani ibada ya arusi ya watu wengi pamoja. Matayarisho yataanza mwezi wa tano.



**Mradi wa Jukua**

***Other Anniversaries in Year 2022***

**Bishop Joseph Mbatia**
- 10 Years of Episcopal Ordination (since 2012)

**Sisters Servants of the Visitation**
- 20 Years of Sisters Community at Ol Moran (since 2002)

**Fr. Giacomo Basso**
- 15 years as a Parish Priest of Ol Moran (since 2007)
- 20 years of Priesthood (since 2002)





*Picha kubwa juu:*
Viongozi, Makatekista na Wakristu wengine tarehe 1 Januari, baada ya ibada ya kukumbuka mwanzo wa Parokia na kuubariki Mwaka Mpya.

*Katikati:*
Wakristu wa Ndunyuriwo, siku ya Semina ya Silver Jubilee, Jumapili 20 Machi

*Chini:*
Fr. Giovanni Volpato alipokaribishwa Ol Moran, mwaka 1997, Parokia ilipoanza.

**PRIESTS WHO SERVED AT OL MORAN**

***Parish Priests***
Fr. Giovanni Volpato (Jan. 1997 - Dec. 2008)
Fr. Giacomo Basso (since Dec. 2008)

***Assistant Parish Priests***
Late Fr. Sebastian Gathogo (Feb. 2009 - Feb. 2014)
Fr. David Kinyanjui (May 2012 - May 2014)
Fr. Samuel Wainaina (May 2014 - May 2015)
Fr. Paul Ngure (Aug. 2015 - Apr. 2017)
Fr. Peter Kinyua (Apr. 2017 - Nov. 2020)
Fr. Simon Ngatia (since Dec. 2020)

***Priests from Ol Moran***
Fr. Paul Maina (ordained in 2002, Maralal Diocese)
Fr. John Maina (ord. in 2015, Nyahururu Diocese)

***Missionary Priests from Padua who served at Ol Moran before being a Parish***
Fr. Luigi Paiaro (Nyahururu Parish)
Fr. Sandro Borsa (Ng'arua Parish)
Fr. Raffaele Coccato (Ng'arua Parish)

# Maendeleo ya Elimu Bora

## Tumaini Academy

KCPE - Hata Shule ya Msingi ya Parokia 'Tumaini Academy' imemaliza mwaka wa Shule na mtihani wa KCPE tarehe 11 Machi. Matokeo yamekuwa mazuri hata kama mwaka uliopita ulikuwa na changamoto ya Corona na ya vita mwezi wa tisa.

NEW H/T - Mwanzo wa Januari, Tumaini Academy ilipata Mwalimu Mkuu mpya, bw. James Waraga. Mwalimu aliweza pia kukutana na wazazi wa wanafunzi Ijumaa 18 Februari.

SCHOOL VAN - Tumaini ilipata pia gari la shule linalosaidia wanafunzi kurahisisha safari ya kufika shuleni na kurudi nyumbani.

CBC - Shule imeendelea kufunza walimu mbinu mpya ya elimu inayoitwa CBC. Masomo ya CBC yashaanza hadi darasa la sita. Pia, shule imeshaanza kupanga masomo ya Junior Secondary, itakayoanza mwaka 2023.

DEVELOPMENT - Kazi ya kujenga bweni la wavulana na ukumbi mkuu wa shule imeendelea sana na inatarajiwa kukamilika mwezi wa saba. Shule imeongeza hata usalama ikijenga ua la mashamba yote ya shule, pia iliweza kupata msaada wa County na kuchimbuliwa barabara kuzunguka shule yote.

DAY CARE - Muhula uliopita ulianza pia huduma ya shule kwa ajili ya watoto wa umri chini wa miaka 3. Masomo ya *Pre-Nursery* (au *Day Care*) yanaendelezwa na walimu wa Tumaini, ijapokuwa yanafanywa Parokiani, kwenye chumba cha Hekima House. Day Care itaanza tena muhula ujao, Jumatatu 25 Aprili.

IRP - Wakati wa likizo wa mwezi wa tatu, shule ilipanga masomo kwa ajili ya wavulana waliofanyiwa tohara, pia wasichana wa umri huo baada ya darasa la nane. Ndio mpango wa *Initiation and Rites of Passage*. Siku ya kuhitimu ilisherehekewa Jumapili 27 Machi, kanisani Ngare Narok.

NEW TERM - Muhula mpya utaanza Jumatatu 25 Aprili, kwa wanafunzi wote, *Day* na *Boarding*.

***Tumaini KCPE 2021-2022***

- *Candidates:* ***33 Pupils***
- *Top Pupils:* ***376, 368, 356 marks***
- *Main Score:* ***309.09***
- *Above 300 marks:* ***20 Pupils***
- *Below 300:* ***12 Pupils***
- *Below 250:* ***1 Pupil with 247 marks***



*Juu:* Maendeleo ya mijengo ya Tumaini Academy

*Chini:* Mwalimu Waraga na gari la shule



## Hekima House

KCSE - Wanafunzi wa kidato cha 4 walimaliza mtihani wao katika Shule ya Upili ya Ol Moran mwanzoni mwa Aprili, na wakaondoka.

HOUSE TRIP - Wanafunzi wote wa Hekima walipata nafasi nzuri ya safari ya Nyumba kwenda katika Lake Nakuru National Park, Alhamisi 3 Machi, kabla ya kufunga shule.

IN-TAKE - Mwezi huu wa Aprili, umeshaanza wakati wa wanafunzi wapya kujiandikisha katika Hekima House kwa muhula mpya. Ombi la kuingia linapokelea katika Ofisi ya Parokia.

NEW TERM - Nyumba itafunguliwa Jumatatu 25 Aprili, Shule ya Upili itaanza masomo tarehe 26.



*Juu:* Safari ya Wanafunzi wa Hekima House

*Chini:* Ujenzi wa Madarasa ya Dam Mbili



## School Support Program

Mradi wa Parokia kwa ajili ya maendeleo ya shule (SSP: *School Support Program*) unaendelea hata mwaka huu. Inasimamia miradi ya Tumaini Academy na Hekima House, pia SSP inaendeleza kazi nyingi nyingine kwa ajili ya elimu katika eneo letu. Mradi huu uliweza kusaidiana na ufadhili wa karo ya shule kwa ajili ya wanafunzi kadhaa katika Shule za Upili za Mithuri na Ol Moran.

SSP ilisaidia Shule ya Msingi ya Ngoisusu kuongeza madarasa mawili ya mabati. Madarasa yaliombewa baraka Jumapili 13 Machi, lakini sherehe ya kufunguliwa rasmi inapangwa na wazazi kwa muhula ujao.

Pia, kazi ya ujenzi wa madarasa mawili ya kudumu inaendelea katika Shule ya Msingi ya Dam Mbili, iliyo Shule ya Serikali inayofadhiliwa na Parokia (*Catholic Sponsored*).

*Shemasi Boguś, kutoka Venisi*

# Huduma ya Shemasi

Mwezi wa kwanza, Shemasi Bogumił Piotr Wasiewicz alitumwa na Askofu Mkuu wa Jimbo la Venisi katika Parokia ya Ol Moran kwa ajili ya huduma ya kishemasi, akijitayarisha kwa ajili ya Sakramenti ya Upadrisho. Shemasi Boguś alizaliwa na kulelewa katika nchi ya Poland, kule Ulaya Kaskazini. Alisoma katika Seminari Kuu ya Venisi, akawa Shemasi tarehe 7 Novemba 2021. Atahudumu hapa Ol Moran mpaka mwanzo wa mwezi wa tano, atakaporudi Italia. Anatarajiwa kufanywa Padri mwezi wa Juni mwaka huu.



*Kushoto:* Shemasi Boguś katika huduma ya baraka ya familia, alipotembelea maboma ya Kanisa la Ol Moran.

## Kumbukumbu ya Francis na Bernard

*Mwezi uliopita Parokia ilipatwa na msiba mkali kwa sababu ya kifo cha ndugu zetu Francis Njenga Ngaruiya na Bernard Wambui Ndung'u.*

*Francis na Bernard walikufa katika ajali, kule Mithuri, kwenye barabara kuu Sipili-Ol Moran, jioni ya Jumatatu 28 Februari. Ibada ya Mazishi yao iliadhimishwa Jumatatu 7 Machi. Wote wawili wakumbukwa kwa sababu ya urafiki wao na kila mtu, na kazi nyingi katika Parokia na eneo letu.*

*Francis Njenga, umri wa miaka 31, alizaliwa Gathanji. Alikuwa Katekista Mkuu wa Ol Moran, mfanyakazi wa Parokia katika Ofisi na Sakristi, Patron wa vijana na kiongozi wa Maskauti wa Parokia.*

*Bernard Ndung'u, umri wa miaka 26, alizaliwa Ol moran. Alikuwa kiongozi wa Vijana na wa Maskauti katika Parokia.*

*Jumatatu 4 Aprili, Wakristu walikusanyika tena pamoja na familia zao kwa kumbukumbu ya mwezi mmoja baada ya kifo, kule Mithuri, ilipotokea ajali yao. Walifanya Misa ya kuwaombea marehemu, kisha kando ya barabara walipanda msalaba na miti miwili ya kuwakumbuka marehemu.*

*Mungu awape amani ya milele!*





*Jimbo Katoliki la Nyahururu*

# Sherehe ya Jimbo na Upadrisho

Jimbo letu la Nyahururu, lilioanzishwa tarehe 25 Machi mwaka 2003, lilifanya Sherehe ya Miaka 19 Jumamosi 26 Machi 2022.

Siku hiyo walisherehekewa pia Askofu Mstaafu Luigi Paiaro, kwa sababu ya miaka 19 ya uaskofu, na Baba Askofu Joseph Mbatia, kwa sababu ya miaka 10 ya uaskofu na uongozi wa Jimbo.

Katika Sherehe hiyo, Jimbo limebarikiwa pia na Mapadri wapya wawili na Mashemasi wapya watatu.

Mapadri wapya ni Fr. Henry Njuguna, kutoka Parokia ya Dondori, na Fr. James Nderitu, kutoka Parokia ya Muhotetu.

Mashemasi wapya ni Deac. Emilio Wachira (Pondo), Deac. Gideon Maina (Shamata) na Deac. Martin Mukuri (Pondo).

Katika Jimbo, yanaendelea maandalizi ya Harambee itakayofanywa mwezi wa sita kwa ajili ya mradi wa Jimbo, yaani ujenzi wa nyumba za kukodesha kule Ol Kalou.

Tena, hata Jimbo letu lilianza masomo na kazi za Sinodi, inayoendelea katika Kanisa lote duniani, kwa amri ya Papa Fransisko.

Kila Parokia imepewa maswali ya Sinodi (*Questionnaire*), kuchangia kimawazo maendeleo ya Kanisa la kisasa.

Synod 2021 2023
For a synodal Church
communion | participation | mission

*HABARI FUPI*

## Vijana

Imeendelea Registration ya Vijana wa Parokia katika Jimbo la Nyahururu. Jumapili ya Matawi, tarehe 10 Aprili, kutakuwa na siku ya Nadhiri wa Vijana waliojiandikisha. Siku hiyo watakuwa hata na Sherehe ya kuwakaribisha vijana wapya (Junior Youth), yaani wavulana na wasichana waliomaliza darasa la nane.

Vijana watakuwa tena pamoja kwa ajili ya Semina ya Siku Tatu Kuu za Pasaka (*Easter Seminar*), kuanzia Alhamisi Kuu, tarehe 14 Aprili, kuanzia saa sita, hadi Jumapili ya Pasaka asubuhi, tarehe 17 Aprili. Semina hiyo ni nafasi ya pekee ya kufuatilia pamoja ibada za Pasaka, pia kupata masomo ya kiimani na kimaisha.

Mwezi uliopita, Jumamosi 12 Machi, viongozi wa Vijana wa kila Kanisa Dogo pamoja na Patrons na Matrons walikutana kwa ajili ya kupanga kazi za mwaka huu na kwa kuchagua Kamati mpya (Youth Executive).

## Kazi za PMC

Watoto wa PMC wa Dekania ya Ng'arua walifanya Charitable Day hapa Ol Moran Jumamosi 26 Februari, wakiwatembelea watoto wa Nyumba ya Magnificat, inayoendelezwa na Masista wetu. Siku hiyo walianza na ibada ya Misa Kanisani iliyongozwa na Fr. Joseph Kagotho, PMC Chaplain wa Ng'arua, kisha walikutana na watoto wa Magnificat, wakiwasaidia na zawadi zao.

Registration ya PMC ya mwaka huu inaendelea. Watoto waombwa kujiandikisha katika kikundi cha PMC katika Makanisa Madogo.

Semina ya Promoters wa PMC wa Jimbo imefanywa Alhamisi 7 hadi Jumamosi 8 Aprili, kule Ol Joro Orok.

## Nadhiri za CMA na CWA

Wanachama wa CMA (*Catholic Men Association*) na CWA (*Catholic Women Association*) watafanya Nadhiri za mwaka pamoja, siku ya Silver Jubilee, tarehe 30 Aprili, katika Misa ya Baba Askofu. Kila Chama kimeanza kujitayarisha kwa Nadhiri kwa njia ya masomo na maombi: Semina ya CWA tarehe 20 Aprili, na Semina ya CMA tarehe 21 Aprili.

## Choir: Mazoezi na Masomo

Wanakwaya wa Parokia wameshaanza kujiandaa kwa ajili ya nyimbo za Ibada ya Sherehe ya Silver Jubilee.

Pia, wanakwaya 12 walikwenda kuhudhuria masomo ya nyimbo ya Jimbo (*Singing Together*) kuanzia Jumapili 3 Aprili.

## Maskauti wafunzwa na KDF

Maskauti wapya wa Parokia walipata masomo ya msingi wa chama (*ITC, Introductory Training Course*) mwisho wa Januari. Mwezi ujao watapanga sherehe ya Investiture na kazi nyingine za muhula mpya. shule zikifunguliwa tena.

Ya pekee yalikuwa pia yale masomo ya *First Aid* na mawaidha ya kimaisha Maskauti waliyopewa na Maofisa wa Jeshi (KDF) pamoja na Kenya Police, Jumamosi 26 Februari, shuleni Tumaini Academy.

## Seminarian Lawrence ahitimu

*Mseminarista Lawrence Thiong'o atakuwa na Sherehe ya kuhitimu katika masomo ya Seminari Kuu ya Falsafa ya Mt. Augustino ya Mabanga, Bungoma, Ijumaa 6 Mei 2022. Sherehe itaanza na ibada ya Misa itakayoongozwa na Kadinali John Njue, katika uwanja wa Seminari kule Bungoma, saa 9.30am.*

*Parokia inapanga safari ya kwenda kushuhudia hatua hiyo muhimu na kumsherehekea Seminarian wetu.*

*Walio na lengo la kujiunga katika safari hiyo, waweza kujiandikisha kwa Coordinator wa Parokia, Mr. Zakayo, ama kwa Coordinator wa Local Church.*

### UTARATIBU WA APRILI 2022

*Jumapili 10 Aprili* - Dominika ya Matawi na Mateso ya Bwana
***Mwanzo wa Juma Kuu***
*Tazama Utaratibu wa Ibada za Juma Kuu katika The Echo, uk. 2*

*Jumapili 17 Aprili* - **Dominika ya PASAKA YA UFUFUKO** *(Yoh 20:1-9)*
*Mwanzo wa Kipindi cha Pasaka (hadi Pentekoste, tarehe 5 Juni)*
→ Misa - 9am: Gituamba, Magadi, Kahuho; 11am: Ol Moran, Bogani.
→ 4.00pm: Ol Moran, Masifu ya Jioni na Baraka ya Kiekaristi

*Jumapili 24 Aprili* - Dominika ya 2 ya Pasaka *(Yoh 20:15-20)*
→ Misa - 7am: Kabati; 9am: Mbombo, Dam Mbili;
10.30am: Nakwang; 11am: Ol Moran; 12noon: Ndunyuriwo.

*Jumatatu 25 Aprili* - *Sikukuu ya Mt. Marko Mwinjili*
→ 7am: Ol Moran, Misa ya Sikukuu

*Jumamosi 30 Aprili* - **Sherehe ya SILVER JUBILEE ya Parokia**
→ 9.30am: Ol Moran: Mwanzo wa Sherehe (taz. Utaratibu uk. 2)

*Jumapili 1 Mei* - Dominika ya 3 ya Pasaka *(Yoh 21:1-19)*
***Mwanzo wa Mwezi wa Bikira Maria***
→ Misa - 7am: Ol Moran; 9am: Magadi, Ngare Narok, Gituamba;
11am: Ol Moran, Lounyek.

*Jumamosi 7 Mei*
→ 10am: Ol Moran, Mkutano wa Makatekista wote.

*Jumapili 8 Mei* - Dominika ya 4 ya Pasaka *(Yoh 10:27-30)*
→ Misa - 7am: Ol Moran; 9am: Kahuho, Ol Motunyi, Miharati;
11am: Ol Moran, Bogani.

***Waumini waliofariki dunia mwezi uliopita:***

28/02: Francis Njenga Ngaruiya (Gathanji) na Bernard Wambui Ndung'u (Ol Moran) | 11/03: Jane Mungore King'atia (Survey) | 23/03: Charles Kinyua (Githima) | 29/03 Michael Ndegwa Kinyanjui (Kabati)

SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO
*- No. 84, Year 14, Printed on 7th April 2022 - (NOT FOR SALE)*
**SAINT MARK** CATHOLIC PARISH - Ol Moran - *Catholic Diocese of Nyahururu*
*P.O.Box 20 - 20320 Kinamba - saintmark@olmoran.it - +254 720 924 153*